

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 49 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** MACHI 2025

WALIMU WATAKIWA KUOMBA USHAURI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI YANAYOHUSU UTUMISHI WAO



*Mwenyekiti
wa Tume ya
Utumishi wa
Walimu (TSC),
Prof. Masoud Hadi
Muruke akizungumza
katika mkutano wake na
walimu wa Wilaya ya
Mafia uliofanyika katika
Ukumbi wa Mikutano
wa Halmashauri ya
Wilaya ya Mafia terehe
25 Februari, 2025.*

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

WATUMISHI SAIDIENI KUIFANYA TSC KUWA KIMBILIO KWA WALIMU

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke alikaririwa akiwataka watumishi wa TSC kote nchini kuhakikisha wanaifanya Tume hiyo kuwa kimbilio kwa walimu kwa kutoa huduma bora.

Ni ukweli usiofichika kuwa watumishi wa Tume wana nafasi kubwa kufanya TSC iwe na taswira njema kwa wadau wake kulingana na namna wanavyohudumia wateja wanaohitaji huduma.


Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imejikita katika kuhakikisha

walimu wanakuwa na mazingira mazuri ya utendaji kazi ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zao.

Hivyo, ili kukamilisha azma hiyo, kila mtumishi wa TSC anapaswa kuwajibika ipasavyo kwa kutekeleza majukumu yake kwa bidii, weledi, ubunifu na uadilifu. Tabia za lugha chafu, rushwa, kutojali na kujifanya miungu watu zinapaswa kuepukwa na kukemewa vikali.

Walimu wanapofika ofisi ya TSC wanapaswa kupata faraja, ushauri, elimu na ufumbuzi wa changamoto zao, hapo ndipo tutakuwa na mchango katika kuunga mkono juhudi za Rais Samia za kuboresha sekta ya elimu na walimu.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

WALIMU WATAKIWA KUOMBA USHAURI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI YANAYOHUSU UTUMISHI WAO



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza katika mkutano wake na walimu wa Wilaya ya Mafia uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari, 2025.

Na Mwandishi wetu – Mafia.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke amewataka walimu nchini kutafuta ushauri sahihi wakati wanapotaka kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu utumishi wao ikiwemo suala la kujiendeleza kielimu.

Prof. Muruke ametoa kauli hiyo katika mkutano wake na walimu wa shule za msingi na sekondari wa Wilaya ya Mafia uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya hiyo tarehe 25 Februari, 2025.

Alisema kuwa kabla ya Mwalimu kwenda kusoma ni muhimu ajue kile anachokwenda kusomea na namna kitakavyomsaidia katika maendeleo ya utumishi wake, kuelewa wakati sahihi wa kwenda kusoma pamoja na kuelewa mabadiliko yanayoweza kutokea katika masuala yake ya kiutumishi ikiwemo kubadilishiwa muundo na kupanda cheo.

“Wapo baadhi ya walimu wanakwenda kusoma lakini ukiangalia unaona wamekosa ushauri sahihi wa kile wanachopaswa kusomea. Mwalimu kama unataka uendelee kukua katika kada yako ni lazima ukajiendeleze katika masuala ya ualimu. Ukifanya hivyo una uhakika kuwa ukimaliza masomo na kwa kuzingatia taratibu

utabadilishiwa cheo. Lakini unakuta mwalimu amejieleza katika fani nyingine mwisho anakuja TSC anataka abadilishiwe cheo, hilo haliwezekani,” alisema.

Aliongeza kuwa, walimu hawana sababu za kutopata ushauri sahihi kwani Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu zipo kwa ajili ya kuwasaidia kufanya maamuzi yenye faida katika utumishi wao.

Mbali na hayo, Mwenyekiti huyo alieleza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo mengi katika Sekta ya Elimu ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kuboresha maslahi ya walimu lengo likiwa ni kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu inayotarajiwa.

Prof. Muruke alisisitiza kuwa dhamira ya Rais Samia ni kuona kila mwalimu anadumu katika ajira na kuteleza majukumu yake kikamilifu, hivyo alitaka ofisi ya TSC Wilaya kutoa ushauri nasaha kwa walimu pale kunapoonekana viashiria vya ukiukaji wa maadili ili kumrekebisha kabla ya kufikia hatua ya kumfungulia shauri la nidhamu.

“Sisi TSC lazima tuelewe kuwa kuwepo kwa mashauri mengi ya nidhamu sio kigezo cha kuonesha kuwa tunafanya kazi vizuri. Mashauri yakiwa mengi kwetu siyo mafanikio, mafanikio yetu ni kuona walimu wanazingatia maadili ya kazi na mashauri yanapungua au yanakwisha

kabisa,” alisema Mwenyekiti huyo.

Kwa Upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama aliwataka walimu kusoma, kuelewa na kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayosimamia utumishi wao ili kutekeleza wajibu wao kwa kuzingatia maadili ya kazi, kuelewa haki zao na taratibu za kuzingatia katika kupata haki hizo.

Pia, aliwaeleza walimu hao ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoe wakati akizindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023 ambapo aliahidi kuwa serikali itapitia upya maslahi ya kada ya walimu ili kuipa hadhi inayostahili kama mama wa taaluma zote duniani.

“Sote Tumemsikia Rais wetu namna anavyojali kada hii ya ualimu, pia tumeona namna anavyopambana kuhakikisha anatatua changamoto mbalimbali ikiwemo upandishwaji vyeo, madai ya malimbikizo ya mishahara, likizo na uhamisho. Tuna kila sababu ya kumshukuru kwa kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kwa bidii,” alisema Mwl. Nkwama.

Aidha, Katibu huyo aliwasihi walimu kuridhika na mazingira ya kazi na kujikita katika kutoa huduma kwa wanafunzi badala ya kuhangaika kutafuta uhamisho ili waondoke katika wilaya hiyo huku akisisitiza kuwa Serikali inaendelea kufanya jitihada za kuweka mazingira bora zaidi ya usafiri kati ya kisiwa hicho na maeneo mengine.

“Tumesikia kuwa kuna baadhi ya walimu wapo Mafia lakini mawazo yao hayapo huku kabisa. Yaani wamejiegasha tu, wala hawataki kuweka makazi ya moja kwa moja ni kama wanasubiria tu kuwa muda wowote wataondoka. Hii inaondoa utulivu wa mwalimu katika kutoa huduma bora ya kufundisha wanafunzi,” alisema Mwl. Nkwama.

Kwa upande wa walimu, walimshukuru Mwenyekiti wa Tume pamoja na ujumbe wake kwa kuwatembelea huku wakieleza kuwa Mafia bado kuna upungufu wa walimu hivyo, Serikali iendelee kutoa kipaumbele kwa Wilaya ya Mafia wakati wa kupangia walimu vituo vya kazi.

WALIMU WATAKIWA KUOMBA USHAURI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI YANAYOHUSU UTUMISHI WAO



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza katika Mkutano wa Walimu wa Wilaya ya Mafia uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya hiyo tarehe 25 Februari, 2025.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifurahia wimbo alioimba na walimu walioshiriki Mkutano uliowakutanisha na Mwenyekiti wa TSC tarehe 25 Februari, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mafia, Bi. Zaituni Sing'ombe akitoa neno la utangulizi wakati wa Mkutano wa Walimu wa Wilaya ya Mafia uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya hiyo tarehe 25 Februari, 2025.



Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Mafia, Mwl. Matheru Mkali akitoa taarifa ya namna Serikali inavyoshughulikia masuala ya walimu katika Mkutano wa Walimu wa Wilaya ya Mafia uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya hiyo tarehe 25 Februari, 2025.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo TSC akiwasalimua walimu waliohudhuria Mkutano wa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari 2025.



Mmoja wa walimu waliohudhuria Mkutano wa Mwenyekiti wa TSC na Walimu wa Wilaya ya Mafia akitoa mchango wake wakati wa mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari, 2025.

WALIMU WATAKIWA KUOMBA USHAURI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI YANAYOHUSU UTUMISHI WAO



Mmoja wa walimu waliohudhuria Mkutano wa Mwenyekiti wa TSC na Walimu wa Wilaya ya Mafia akitoa mchango wake wakati wa mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari, 2025.

Mmoja wa walimu waliohudhuria Mkutano wa Mwenyekiti wa TSC na Walimu wa Wilaya ya Mafia akitoa mchango wake wakati wa mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari, 2025.



Walimu Waliohudhuria Mkutano wakizwa kwenye mkutano huo uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari, 2025.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu walioshiriki mkutano wake na walimu wa Wilaya ya Mafia tarehe 25 Februari, 2025. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama pamoja na viongozi wengine.

WALIMU WATAKIWA KUOMBA USHAURI KABLA YA KUFANYA MAAMUZI YANAYOHUSU UTUMISHI WAO





OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Ramadhan

Karëëm

M u b a r a k

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
Tunawatakia Waislamu wote mfungo
mwema wa Mwezi Mtukufu
wa Ramadhani



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

WAJUMBE WA TSC WAKUTANA KUPITIA NA KUAMUA RUFAA ZA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Morogoro.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inafanya Mkutano wake wa kisheria mjini Morogoro ambao umelenga kujadili na kuamua masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu nchini.

Mkutano huo wa siku tano (5) ulioanza tarehe 10 Februari, 2025 ulifunguliwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Masoud Hadi Muruke ambapo pamoja na mambo mengine utapitia na kutoa uamuzi wa rufaa 22 za walimu ambao wamepinga uamuzi uliotolewa na TSC ngazi ya wilaya katika mashauri yao ya kinidhamu.

Akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa kikao hicho, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa walimu (7) kati ya 22 ambao rufaa zao zitaamuliwa wameomba kufika mbele ya tume ili waweze kutoa maelezo ya ziada yanayohusu rufaa zao.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa sanjari ya hilo Wajumbe watapitia maombi ya walimu 23 walioomba kuajiriwa upya katika Utumishi wa



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akifungua Mkutano wa Tume tarehe 10 Februari, 2025 mjini Morogoro. Wengine katika picha ni Makamu Mwenyekiti, Bi Mariam Mgongolwa (kulia) na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama.

Umma baada ya kutumikia adhabu ya kufukuzwa kazi kwa zaidi ya miezi 12.

Vilevile, Mkutano huo unatarajiwa kuteua wajumbe wa Kamati ya TSC

kwa ngazi ya Wilaya katika Ofisi 17 ili kujaza nafasi zilizoachwa wajumbe walipoteza sifa za kuendelea na nafasi hizo kutokana na sababu mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016.

Mkutano huo ulitanguliwa na vikao vya Kamati tatu (3) za Tume ambazo ni Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma na Kamati ya Maadili na Nidhamu ambapo taarifa za Kamati hizo ni miongoni mwa agenda za kujadiliwa katika Mkutano wa Tume.

Katika hatua nyingine Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wameiagiza Menejimenti ya Tume inawapanga Maafisa kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu na Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu watakuwa viungo na watumishi wa Tume katika Ofisi za TSC ngazi za Wilaya na hivyo kuimarisha mawasiliano na kurahisisha utendaji wa kazi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa TSC uliofanyika tarehe 10 Februari 2025 mjini Morogoro. Wengine katika picha ni Mwenyekiti wa Tume, Pro. Maoud Hadi Muruke (katikati) na Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi Mariam Mgongolwa (kulia).

WAJUMBE WA TSC WAKUTANA KUPITIA NA KUAMUA RUFAA ZA WALIMU



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Nidhamu ya TSC, Mv. Jane Mtindya akiwasilisha taarifa ya kamati yake kwenye Mkutano wa Tume tarehe 10 Februari, 2025 mjini Morogoro.



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma na Kamati ya Maadili na Nidhamu ya TSC, Bw. Agrey Mleli (mbele Katikati) akiwasilisha taarifa ya Kamati hiyo kwenye Mkutano wa Tume tarehe 10 Februari, 2025 mjini Morogoro.



Kamishna na Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya TSC, Mwl. Lameck Mahewa akiwasilisha taarifa ya Kamati hiyo kwenye Mkutano wa Tume tarehe 10 Februari, 2025 mjini Morogoro.



Kamishna na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bi. Mariam Haji (wa kwanza kulia) akiwa katika Mkutano wa Tume hiyo.



Baadhi ya Washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika mkutano huo tarehe 10 Februari, 2025.

WAJUMBE WA TSC WAKUTANA KUPITIA NA KUAMUA RUFAA ZA WALIMU



Baadhi ya Washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika mkutano huo tarehe 10 Februari, 2025.



Washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika mkutano huo tarehe 10 Februari, 2025.

WATUMISHI WA TSC WATAKIWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Kibiti.

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wametakiwa kutoa huduma bora kwa wateja hususan walimu ili ofisi za TSC kote nchini ziwe kimbilio pale wanapohitaji kupata huduma.

Agizo hilo limetolewa na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke wakati akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kibiti pamoja na watumishi wa TSC wa Wilaya wakati wa ziara yake aliyoifanya katika ofisi hiyo tarehe 26 Februari, 2025.

Alisema kuwa watumishi wa TSC wanapaswa kuwa na lugha nzuri, kutoa elimu na ushauri kwa walimu katika masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wao na kuepuka kuweka matabaka kati yao na walimu.

Aliongeza kuwa TSC itaendelea kuwa kimbilio endapo tu walimu wataona wanapata ufumbuzi wa changamoto zao kwa upendo, kuheshimiwa na kuthaminiwa hivyo aliwataka watumishi wenye tabia ya kutowajali walimu kuacha tabia hiyo mara moja.

“Walimu wetu wameendelea kutuamini kwa kuwa tunawahudumia vizuri, tuendeleo hivyo. Hata hivyo, kuna baadhi ya watumishi wachache kwenye ofisi zetu wanaoonekana kuwa miungu watu, wana viburi, wanatoa lugha chafu na kuwafokea walimu, tabia hiyo tatuwezi kuikubali hata kidogo,” alisema Prof. Muruke.

Aliongeza kuwa, “Unakuta mwalimu anafika ofisini kwako hata hujamsikiliza unaanza kumshambulia kwa maneno makali mpaka anakosa uhuru wa kuwasilisha shida yake. Tunapaswa kuelewa kuwa ofisi hizi tumepewa dhamana ili kuwapa amani walimu na sio kuwa kero kwao.”

Vilevile, Mwenyekiti huyo alisisitiza kuwa TSC haipaswi kukaa tu na kusubiri kuwachukulia hatua za kinidhamu walimu wanaokwenda

kinyume na maadali ya kazi na badala yake wanapaswa kutoa elimu na ushauri ili wasikiuke maadili ya kazi.

“TSC tusijulikane kwa mashtaka tu. Walimu wetu wanahitaji kupewa elimu na kukumbushwa mara kwa mara juu ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayohusu utumishi wao. Kuna wengine wanakiuka maadili kwa kutokujua taratibu, hivyo ni lazima tuwasaidie waepuke kutenda makosa,” alisisitiza.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama lipongeza Ofisi ya TSC Kibiti kwa kutekeleza majukumu yao vizuri huku akionesha kuridhishwa na ushirikiano uliopo kati ya ofisi hiyo na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

“Niwapongeze kwa kazi nzuri mnayoifanya katika kuwahudumia walimu. Pia, tunamshukuru Mkurugenzi kwa kuwapatia vyumba vya ofisi kwenye jengo hili la Halmashauri. Hii inaonesha kuwa kuna ushirikiano mzuri kati yetu na Ofisi ya Mkurugenzi,” alisema.

Mwl. Nkwama alielekeza watumishi wa TSC wa Wilaya hiyo kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kwamba walimu ambao bado wana changamoto mbalimbali zikiwemo madeni ya likizo, uhamisho, malimbikizo ya mishahara, kucheleweshwa kubadilishiwa kazi/cheo na kucheleweshwa kupanda cheo wanatatuliwa changamoto hizo.

Alifafanua kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele katika kuboresha elimu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha walimu wanapata haki zao kikamilifu ili waweze kutoa huduma bora katika kufundisha wanafunzi.

“Kwenye taarifa nimesikia kuna maombi 11 ya walimu wanaoomba kubadilishiwa kazi/cheo, kuna malalamiko 54 yanayohusu upandishwaji vyeo pamoja na changamoto za madeni ya walimu. Fanyeni ufuatiliaji wa karibu na Ofisi ya Mkurugenzi kuhakikisha changamoto



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza na Wajumbe wa Kamati pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti tarehe 26 Februari, 2025 kwenye kikao kilichofanyika kwenye Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

hizo zinatatuliwa kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa,” alielekeza.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utendaji wa kazi ya Ofisi yake, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kibiti, Bw. Ali Masoud alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 walimu 509 walipandishwa vyeo ambapo walimu wa shule za msingi walikuwa 351 na sekondari wakiwa 184 huku walimu 25 wakibadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza kielimu na kukidhi vigezo.

“Hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya mashauri 12 ya walimu yalifunguliwa ambapo mashauri 10 yamehitimishwa. Mashauri hayo yalihusu makosa ya matumizi mabaya ya mamlaka, utoo kazini na ukiukwaji wa utendaji wa maadili ya utendaji kazi ya ualimu,” alisema.

Bw. Masoud alisema Wilaya hiyo ina jumla ya shule 107 za serikali, kati ya hizo 88 ni za msingi na 19 ni za sekondari huku ikiwa na jumla ya walimu 892, kati ya hao 602 ni wa shule za msingi na 290 ni wa shule za sekondari.

WATUMISHI WA TSC WATAKIWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na Wajumbe wa Kamati pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti tarehe 26 Februari, 2025 kwenye kikao kilichofanyika katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.



Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibiti, Mwl. Fredrick Mchome akisalimia wakati wa kikao cha Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke (hayupo pichani) na Wajumbe wa Kamati ya Wilaya pamoja na Watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2025 katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibiti, Bw. Ali Masoud akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo wakati wa kikao cha Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke (hayupo pichani) na Wajumbe wa Kamati ya Wilaya pamoja na Watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2025 katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Fatuma Muya wakifuatilia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya ya Kibiti kwenye kikao kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2025 katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti.

WATUMISHI WA TSC WATAKIWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



Kaimu Mkurugenzi wa Seksheni ya Maadili na Nidhamu TSC, Mwl. Asha Lubuwa (kulia) akipitia nyaraka wakati wa kikao kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2025 katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti. Pichani, pembeni yake ni Mtumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti, Bi. Adelina Nyoni.

Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibiti, Tatu Kassim Ally (kulia) na Kudra Suleiman wakiwa kwenye kikao kilichowakutanisha Mwenyekiti wa TSC Prof. Masoud Hadi Muruke na ujumbe wake, Kamati ya TSC na watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti tarehe 26 Februari 2025 wilayani Kibiti.

Mjumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibiti, Maria Katemana, akitoa salamu kwenye kikao kilichowakutanisha Mwenyekiti wa TSC Prof. Masoud Hadi Muruke na ujumbe wake, Kamati ya TSC na watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti tarehe 26 Februari 2025 wilayani Kibiti.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo na Watumishi wa TSC Wilaya ya Kibiti tarehe 26 Februari, 2025. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama pamoja na viongozi wengine.

USHIRIKIANO KATI YA TSC NA WADAU WA ELIMU WILAYANI MOMBA WASAIDIA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WALIMU

Na Mwandishi wetu – Momba.

Ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na wadau wa elimu hususan Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma umesaidia kutatua changamoto mbalimbali za walimu katika Wilaya ya Momba.

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Momba, Bw. Ferdinand William wakati akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Tume ya Utumishi wa Walimu waliofika katika ofisi za TSC Momba kwa lengo la kufahamu namna Tume inavyotoa huduma kwa walimu wilayani hapo.

Bw. William alisema kuwa Wilaya ya Momba ina Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Momba na Halmashauri ya Mji Tunduma ambapo changamoto za walimu zimeendelea kushughulikiwa kutokana na ushirikiano ambao Tume inaupata kutoka katika ofisi za Halmashauri hizo.

“Katika kushughulikia masuala ya walimu tunapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa Maafisa Elimu, Maafisa Utumishi pamoja na Wakurugenzi wenyewe. Kwa kushirikiana na Maafisa Elimu, tumefanya ziara mbalimbali na kukutana na walimu kwa lengo la kutoa elimu juu ya masuala ya utumishi pamoja na kusikiliza na kutatua kero zao,” alisema.

Aliongeza kuwa, “Tunafanya vikao vya mara kwa mara na viongozi wanaosimamia elimu ndani ya wilaya ambao ni Maafisa Elimu Kata, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wa Wilaya. Vikao hivi vimetusaidia kushughulikia matatizo ya walimu kwa pamoja na kwa muda mfupi. Pia, tunashirikishwa katika vikao vya elimu vinavyofanyika kwa ngazi ya Mkoa”.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema miongoni

mwa mafanikio ya ushirikiano huo ni kulipwa kwa madeni yote ya walimu wanaosimamiwa na Idara ya Elimu Msingi katika Halamshauri ya Mji Tunduma yakiwemo malimbikizo ya mishahara, likizo na uhamisho yaliyokuwepo kuanzia mwaka 2023/2024 kurudi nyuma.

“Madeni ya walimu wa shule za msingi yaliyokuwepo yamelipwa. Kwa mwaka huu wa 2024/2025 yapo madai machache ambayo nayo malipo yake yatakamiliwa katika kipindi kifupi. Na hata walimu wengine wanaodai wameendelea kulipwa na kwa kuwa nia ya Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha changamoto za walimu zinatatuliwa, wote wenye madai watalipwa,” alisisitiza.

Kutokana na ushirikiano uliopo TSC Wilaya ya Momba imepandisha vyeo walimu 919 katika mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo walimu 460 ni kutoka Halmashauri wa Wilaya ya Momba na Walimu 459 ni kutoka Halmashauri ya Mji Tunduma.

Kwa upande wa nidhamu, Bw. William alisema kuwa kwa kiasi kikubwa walimu katika Wilaya ya Momba wanazingatia maadili ya kazi kutokana na elimu ya mara kwa mara wanayoitoea huku akibainisha kuwa katika mwaka 2023/2024 Walimu wanne (4) walifunguliwa mashauri ya nidhamu na kati ya hao mmoja (1) ndiye aliyepatikana na hatia.

Alisema kuimarika kwa nidhamu kumesaidia kuongezeka kwa uwajibikaji kwa walimu katika kufundisha wanafunzi huku akitolea mfano wa Halmashauri ya Mji Tunduma ambayo katika matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba wa mwaka 2024 wastani wa ufaulu ulikuwa asilimia 95.

Wilaya ya Momba ina jumla ya shule za Serikali 1671 ambapo shule za msingi ni 862 na sekondari ni 809, kwa upande wa walimu wilaya hiyo ina jumla ya walimu 180 wanaohudumiwa na TSC, kati ya hao 110 ni wa shule za msingi na 80 ni wa shule za sekondari.

MWENYEKITI, KATIBU TSC WAFANYA ZIARA MAFIA



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia), Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu ya TSC, Mwl. Fatuma Muya (wa kwanza kulia) na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Asha Lubuva mara baada ya kuwasili Wilayani Mafia tarehe 24 Februari, 2025 katika ziara ya kutemebela Ofisi ya TSC Wilayani Mafia.

Na Mwandishi wetu – Mafia.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke tarehe 24 Februari, 2025 amefanya ziara ya siku mbili katika Ofisi za TSC za Wilaya ya Mafia kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.

Katika ziara hiyo, Prof. Muruke ameambatana na viongozi kutoka TSC Makao Makuu ambao ni Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya pamoja na Mkurugenzi Msaidizi wa Seksheni ya Maadili na Nidhamu, Mwl. Asha Lubuva.

Alipowasili wilayani Mafia, Mwenyekiti wa Tume pamoja na ujumbe wake walipokelewa na Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya ya Mafia ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwl. Shabani Zuberi Shemsanga na kisha kufanya kikao kilichohusisha Kamati hiyo pamoja na watumishi wa

TSC wa Wilaya hiyo.

Akizungumza katika kikao hicho, Prof. Muruke alisema kuwa lengo la ziara ni kuona maendeleo ya TSC katika kutoa huduma kwa walimu ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa walimu inafikiwa.

“Tumekuja Mafia kuona maendeleo ya Tume katika kushughulikia masuala ya kiutumishi ya walimu, namna tunavyotatua changamoto zao, namna tunavyosimamia haki zao lakini pia kuona namna tunavyosimamia uwajibikaji wa walimu katika kutoa huduma kwa wanafunzi,” alisema Prof. Muruke.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama aliwapongeza watumishi wa TSC Wilaya ya Mafia kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kusimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu jambo ambalo limefanya walimu kuendelea kuwa watulivu na kutekeleza majukumu yao kwa bidii na uzalendo.

Pamoja na pongezi hizo, Mwl.

Nkwama aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanazielewa na kuzitumia kwa usahihi Sheria na Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu hususan wakati wa kushughulikia mashuri ya nidhamu ya walimu ili kutenda haki.

Alifafanua kuwa kuna nyakati baadhi ya Ofisi za Wilaya za TSC hufanya dosari kwa kutozingatia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu katika kuendesha mashauri ya nidhamu na kusababisha mashauri kurudishwa kuanza upya pale yanapokatiwa rufaa kupinga uamuzi uliotolewa na TSC ngazi ya Wilaya na hivyo kuisababishia Serikali hasara.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya TSC Wilaya ya Mafia, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume wa Wilaya hiyo, Bi. Zaituni Sing'ombe alisema kuwa Wilaya ya Mafia ina shule za Serikali 45 ambapo kati ya hizo 36 ni za msingi na tisa (9) ni za Sekondari huku ikiwa na Walimu 346 wanaohudumiwa na TSC, kati ya hao 237 ni wa shule za msingi na 99 ni wa shule za Sekondari.

Aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 walimu 50 walipandishwa vyeo na mwaka 2023/2024 walimu 162 walipandishwa huku walimu watano wakibadilishiwa kazi/cheo kwa mwaka 2022/2023 na walimu 32 wakibadilishiwa kazi/cheo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Naye Afisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Mafia, Mwl. Mathew Mkali alisema kuwa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imetatua changamoto mbalimbali za walimu ikiwemo kulipa madai ya likizo, uhamisho na malimbikizo ya mishahara na hivyo kuondoa malalamiko ya walimu yaliyokuwepo muda mrefu.

“.....kwa mfano, kwa upande wa Idara ya Elimu Msingi, tumeongezewa ukomo wa bajeti katika maeneo ya likizo za walimu kutoka milioni 34 hadi milioni 90. Hii imetuwzesha kulipa madeni ya walimu kwa kiasi kikubwa na tunaamini madeni yaliyobaki tutaendelea kuyalipa na hatimaye yatakwishwa,” alisema Mwl. Mkali.

Katika ziara hiyo, Mwenyekiti wa Tume pamoja na ujumbe wake watatemebea Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, Shule ya Msingi Kilimahewa pamoja na kufanya Mkutano na Walimu wa Wilaya hiyo.

MWENYEKITI, KATIBU TSC WAFANYA ZIARA MAFIA



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati), Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Mafia, Bi. Zaituni Sing'ombe wakielekea ofisi za Tume Wilaya ya Mafia kwa ajili ya kufanya kikao.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza katika kikao kilichowahusisha Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya na Watumishi wa TSC Wilaya ya Mafia tarehe 24 Februari, 2025.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza katika kikao kilichowahusisha Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo na Watumishi wa TSC Wilaya ya Mafia tarehe 24 Februari, 2025.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Mafia, Bi. Zaituni Sing'ombe akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wamajukumu ya Tume Wilaya ya Mafia katika kikao cha Mwenyekiti wa Tume na Ujumbe wake pamoja na wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo na Watumishi wa TSC Wilaya ya Mafia tarehe 24 Februari, 2025.

Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu ya TSC, Mwl. Fatuma Muya akichangia hoja wakati wa kikao cha Mwenyekiti wa Tume na ujumbe wake pamoja Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya na Watumishi wa TSC Wilaya ya Mafia tarehe 24 Februari, 2025.

MWENYEKITI, KATIBU TSC WAFANYA ZIARA MAFIA



Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya ya Mafia, Mwl. Shabani Zuberi Shemsanga akichangia hoja wakati Kamati yake ilipokutana na Mwenyekiti wa TSC aliyeambatana na ujumbe wake katika ziara iliyofanyika wilayani humo tarehe 24 Februari, 2025.



Mjumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya na Watumishi wa TSC Wilaya ya Mafia na Afisa Elimu wa Idara ya Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Mwl. Mathew Mkali akichangia hoja katika kikao cha Mwenyekiti wa Tume aliyeambatana na ujumbe wake katika ziara ya kikazi wilayani Mafia tarehe 24 Februari, 2025.



Kikao cha Mwenyekiti wa Tume aliyeambatana na ujumbe wake katika ziara ya kikazi wilayani Mafia tarehe 24 Februari, 2025 kikiwa kinaendelea.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akisaini kitabu cha maombolezo alipofika kuhani msiba wa Alhaji Omari Rashid Mchengerwa, baba mzazi wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) nyumbani kwa Waziri huyo Masaki jijini Dar es Salaam tarehe 26 Februari, 2025.

Prof. Muruke aliambatana na Katibu wa TSC, Mwl.

Paulina Nkwama, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Seksheni ya Maadili na Nidhamu, Mwl. Asha Lubuva pamoja na Afisa Habari wa Tume, Bw. Adili Mhina.

Mwenyekiti na ujumbe wake waliwakilisha Makamishna, Menejimenti na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu.



TSC YAIPONGEZA OFISI YA MKURUGENZI HALMASHAURI YA MAFIA KWA USHIRIKIANO

Na Mwandishi wetu – Mafia.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeipongeza Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia kutokana na ushirikiano inaoutoa kwa Ofisi ya TSC Wilaya ya Mafia katika kutoa huduma kwa walimu.

Pongezi hizo zimetolewa na Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke alipotembelea Ofisi ya Mkurugenzi huyo tarehe 25 Februari, 2025 akiwa katika ziara ya siku mbili wilayani hapo.

“Mafia tunawashukuru sana kwa ushirikiano mnaotupa katika kuhakikisha TSC inatoa huduma kwa walimu bila vikwazo. Tunawashukuru mmetupatia chumba cha ofisi na pia mnatuhusisha kwenye ziara na kazi mbalimbali zinazohusu walimu. Tukiwa na ushirikiano mzuri ni rahisi kushughulikia masuala ya walimu kwa haraka,” alisema Prof. Muruke.

Naye Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama alisema ni muhimu kwa Ofisi ya Mkurugenzi kuendelea kufanya uhakiki wa madeni mbalimbali ya walimu na kuyaingiza kwenye mfumo ili yashughulikiwe na hatimaye walimu wapatiwe haki zao.

“Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele kikubwa katika kushughulikia masuala ya walimu ikiwa ni pamoja na kulipa madeni yao mbalimbali. Hivyo, tunaomba na ninyi muendeleo kufanya uhakiki wa madeni ya walimu na kuwasilisha kwenye mamlaka husika kwa kadiri yanavyojitokeza,” alisema.

Pia, alisisitiza Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kuendelea kushirikiana kwa karibu na TSC ili walimu waliowasilisha maombi ya kubadilishiwa kazi/cheo baada ya kujiendeleza kielimu waweze kushughulikiwa kwa kuzingatia miongozo iliyopo.



Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza wakati wa Kikao na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Bi. Asha Ilelewe kilichofanyika tarehe 25 Februari, 2025 katika Ofisi za Mkurugenzi huyo wilayani Mafia.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza wakati wa Kikao na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Bi. Asha Ilelewe kilichofanyika tarehe 25 Februari, 2025 katika Ofisi za Mkurugenzi huyo wilayani Mafia.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Bi. Asha Ilelewe alimshukuru Mwenyekiti wa Tume pamoja na ujumbe wake kwa kuamua kufanya ziara katika Wilaya hiyo huku akiahidi kuendeleza ushirikiano kati ya TSC na Ofisi ya Mkurugenzi pamoja na kueleza kuwa ofisi yake itaendelea kushughulikia madeni ya walimu kwa nguvu kubwa ili walimu wapate maslahi yao bila vikwazo.

Baada ya mazungumzo hayo, Mwenyekiti wa TSC pamoja na ujumbe wake walipata fursa ya kufanya Mkutano na Walimu wa Wilaya ya Mafia.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Bi. Asha Ilelewe akizungumza wakati alipokutana na Mwenyekiti wa Tume na ujumbe wake tarehe 25 Februari, 2025.

TSC YAIPONGEZA OFISI YA MKURUGENZI HALMASHAURI YA MAFIA KWA USHIRIKIANO



Kikao kati ya Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Fatuma Muya pamoja na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmsahauri ya Mafia, Bi. Asha Ilelewe kikiwa kinaendelea.

MENEJIMENTI YA TSC YAAHIDI KUTOA USHIRIKIANO KWA KAMATI YA UKAGUZI

Na Mwandishi Wetu-Dodoma

Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeahidi kutoa ushirikiano kwa Kamati ya Ukaguzi ya TSC katika wa utekelezaji wa majukumu yake kwa ajili ya kuhakikisha kuwa Taasisi inafanya vizuri katika utoaji wa huduma zake kwa umma.

Kauli hiyo imetolewa tarehe 18 Februari, 2025 na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama wakati akizindua kikao cha Kamati mpya ya Ukaguzi ya TSC kilichofanyika jijini Dodoma.

Alisema kuwa Kamati ya Ukaguzi ina kazi muhimu ikiwemo kutoa ushauri kwa Afisa Masuhuli kuhusu masuala ya uendeshaji wa Taasisi katika maeneo mbalimbali hasa ya usimamizi wa fedha, rasilimaliwatu, manunuzi, vihatarishina na mifumo ya utawala bora.

Mwl. Paulina aliitaka Kamati hiyo kuwa huru katika kutekeleza majukumu yake na kuahidi kuwa Tume iko tayari kutoa ushirikiano wakati wowote kwa kupokea ushauri na maoni ambayo yatasaidia Taasisi hiyo kusonga mbele katika utekelezaji wa majukumu yake iliyopangiwa.

"Nyie ndio jicho letu la kutusaidia, kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa usahihi ikiwemo matumizi ya mifumo mbalimbali kama vile matumizi ya NeST katika manunuzi na usimamizi wa rasilimali watu kwa ajili ya kutuwezesha kutoa huduma zinazotakiwa," alisisitiza.

Mwl. Paulina alisema kuwa Kamati ya Ukaguzi ya Tume iliteuliwa tarehe 9 Januari, 2025 baada ya iliyokuwepo awali kumaliza muda wake huku akieleza kuwa kwa kuwa baadhi ya wajumbe ni wapya mpango wa kuwajengea uwezo unaandaliwa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa weledi zaidi.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya hiyo, CPA Upendo Werema alisisitiza



Kikao cha Kamati ya Ukaguzi ya TSC kilichofanyika tarehe 17 Februari, 2025 jijini Dodoma kikiwa kinaendela.

kuwa umuhimu wa kuzingatia kufanyika kwa vikao kwa wakati ili Kamati itekeleze majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

Aliitaka Menejimenti kuhakikisha kuwa inaendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati mpya kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa manufaa ya TSC.

WALIMU ILEJE WATOA KONGOLE KWA SERIKALI KWA KUWASOGEZEA HUDUMA

Na Mwandishi Wetu – Ileje.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ileje imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inaoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi za kushughulikia kero mbalimbali za walimu ili kuwawekea mazingira mazuri ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wilayani humo.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ileje, Bw. Samwel Chengulah kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ileje wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha TSC.

Bw. Chengulah alisema kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau imesogeza huduma ya kusikiliza kero na changamoto wanazokabiliana nazo kupitia Samia Teachers' Mobile Clinic.

Alisema kuwa kupitia huduma hiyo ya Kliniki iliyosogezwa karibu na walimu na hivyo kusaidia kutotumia gharama kubwa kusafiri huku wakipata fursa nzuri ya kuwasilisha kero zao.

“Walimu wameweza kufikiwa na kuwasilisha changamoto zao za madaraja, muundo na madai mbalimbali na kuwa na imani kubwa ya kuweza kutatuliwa,” alisema.

Bw. Chengulah aliongeza kuwa Uongozi wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umesaidia kushughulikia kero na changamoto za walimu na umeendelea kulipa malimbikizo ya mishahara (Arreas) kwa walimu waliokuwa wakidai kwa muda mrefu.

Bw. Chengulah alisema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu imekuwa ikishirikiana sana na Ofisi za Wakurugenzi kuhakikisha madeni yanayotokana na likizo na mambo mengine kwa mujibu wa Sheria yanalipwa.

Aliongeza kuwa kumekuwa na kasi kubwa ya ulipaji wa madeni ya walimu

hasa ya malimbikizo ya mishahara, ambapo kuanzia mwaka 2017 hadi 2024 walimu 384 wamelipwa madai yao na walimu 80 na wengine madai yao yanaendelea kufanyiwa taratibu ili yaweze kulipwa.

Bw. Chengulah alisema kuwa katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, jumla ya walimu 317 walipandishwa madaraja ikiwa wa Shule za Msingi 211 na Sekondari 106 na kuongeza kuwa walimu wamethibitishwa kazini katika kipindi hicho.

“Pia tunashukuru Serikali kwa kutoa mafunzo ya wajumbe wa Kamati ya Wilaya kwani yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu kwa kuwa na uelewa wa kutosha juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Walimu. Hivyo imewajengea uwezo mkubwa katika kufanya maamuzi kwa kuzingatia taratibu bila ya kutumia utashi binafsi,” alisema.

Bw. Chengulah aliongeza kuwa mafunzo kwa Walimu Wakuu wa Shule yamesaidia kuleta matokeo chanya kwani wamekuwa na uwezo mkubwa wa kutoa elimu kwa walimu wenzao na kushughulikia mashauri mapema kwa kufuata taratibu stahiki kulingana na kanuni na Sheria za Utumishi wa Walimu na kudhibiti masuala ya utovu wa nidhamu kwa walimu.

Aidha, Bw. Chengulah alisema kuwa TSC Wilaya ya Ileje imetembelea shule na kutoa elimu juu ya masuala ya ajira, maadili, nidhamu na haki za kiutumishi ikiwamo kwa Walimu wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata.

Alisema kuwa elimu pia ilisaidia kuwawezesha kutambua mamlaka yao kisheria (Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule) na kuweza kujua namna ya kushughulikia makosa madogo na namna ya kuanzia mchakato wa mashitaka kwa makosa makubwa ya Kinidhamu.

“Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule wameweza kujua na kutambua kuwa wao ni Mamlaka ya Nidhamu katika ngazi ya Shule na kupewa mamlaka na Kanuni 12(3) ya Kusimamia utekelezaji wa majukumu mbalimbali kwa walimu na kutoa adhabu kwa makosa mepesi



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ileje, Bw. Samwel Chengulah akiwa katika mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha TSC (hawapo katika picha) hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali katika kushughulikia changamoto mbalimbali zilizowakabili walimu.

kwa mwalimu aliyekiuka taratibu za kiutumishi,” alisema.

Alisema kuwa wamekuwa wakitembelea shule mbalimbali na kutoa Elimu juu ya masuala ya ajira, maadili, nidhamu na haki za kiutumishi na kutoa Elimu kwa Walimu wakuu na Wakuu wa Shule hasa katika Vikao vyao ili yaweze kutambua mamlaka yao kisheria na kuweza kujua namna ya kushughulikia makosa mepesi na namna ya kuanzisha mchakato wa mashtaka kwa makosa makubwa ya kinidhamu.

Alisema kuwa Wilaya ya Ileje ina jumla ya Shule 110, kati ya shule hizo za msingi ni 88 na za Sekondari ni 22 ambazo zinahudumiwa na walimu 816 ikiwa wa Shule za Msingi ni 516 na Sekondari ni 300.

TSC YAWAKUTANISHA WADAU KUTAFUTA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya kikao kilichowakutanisha wadau mbalimbali wanaohusika katika masuala ya utumishi wa walimu nchini kwa lengo la kujadili masuala yanayoathiri utoaji wa huduma katika utumishi wa walimu ili kupata ufumbuzi wake.

Kikao hicho kilichofanyika tarehe 21 Februari, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma kilifunguliwa na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama ambaye alieleza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu ina dhamira ya dhati ya kudumisha na kusimamia utumishi wa walimu kwa mujibu wa kifungu cha 5(a) cha sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu sura ya 448.

Alisema kikao hicho kinatarajia kutafuta suluhisho la changamoto zinazowakabili walimu katika utumishi wao ikiwemo masuala ya malimbikizo ya mishahara, uhamisho wa mishahara, malipo wa mafao na pensheni na Walimu wa leseni waliojiiriwa bila kuwa na sifa za ualimu.

“Tuna wajibu wa kuhakikisha

kuwa walimu wanapata haki zao kwa wakati, na ni muhimu kutambua kwamba changamoto hizi hazihusishi tu walimu bali pia zinahusiana na maendeleo ya taifa letu. Kwani sote tunakubali kwamba walimu ni mama wa kada zote duniani, wakipata huduma bora na stahiki zao kwa wakati ni dhahiri kwamba watatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na sekta ya elimu itaendelea kuimarika,” alisema Mwl. Nkwama.

Aliongeza kuwa Tume imekuwa ikifanya kazi kwa ushirikiano na Mamlaka au Taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Rais - IKULU, Ofisi ya Rais -UTUMISHI, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Tume ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii - PSSSF, Wakurugenzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, na wadau wengine ikiwemo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mthibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

“Natoa wito kwa kila mmoja wetu kushiriki kikamilifu katika kikao hiki ili tuwe na majadiliano yenye tija na kutoa mapendekezo ambayo yataweza kutatua changamoto hizi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongoza kikao cha wadau wa TSC kilichofanyika tarehe 21 Februari, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Mbele yetu kuna safari ndefu ya kuhakikisha kuwa walimu wanapata huduma bora na kwamba kila mmoja wetu katika sekta hii anafanya kazi kwa ushirikiano na kwa manufaa ya taifa letu,” alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Mwl. Nkwama alitoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza mikakati ya kiuchumi na kijamii ikiwemo kusimamia mazingira ya kazi ya walimu kwa kuhakikisha maslahi ya walimu yanapewa kipaumbele.

Alifanua kuwa katika mwaka 2024/2025 Serikali imetoa vibali vya ajira za walimu 14,648 na katika mwaka 2023/2024 iliwapandisha vyeo walimu 158,916 na kueleza kuwa hatua hiyo itasaidia kupunguza malalamiko, kuongeza tija na ufanisi wa kazi na hivyo kuinua kiwango cha elimu nchini.

Wadau walioshiriki kikao hicho ni pamoja na Ofisi ya Rais -IKULU, Ofisi ya Rais -UTUMISHI, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Tume ya Utumishi wa Umma na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii - PSSSF.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua kikao cha wadau wa TSC kilichofanyika tarehe 21 Februari, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

TSC YAWAKUTANISHA WADAU KUTAFUTA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU



Washiriki wa kikao cha wadau wa TSC kilichofanyika tarehe 21 Februari, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma wakiwa kwenye kikao hicho.



Kikao cha wadau wa TSC kilichofanyika tarehe 21 Februari, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma kikiwa kinaendelea.

KAMATI ZA TSC ZA WILAYA ZATAKIWA KUONGEZA UFANISI WA UTENDAJI KAZI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga wakati wa ziara yake katika Ofisi za TSC za Wilaya hiyo tarehe 27 Februari, 2025.

Na Mwandishi wetu – Mkuranga.

Kamati za Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya kote nchini zimetakiwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika kutoa maamuzi ya masuala mbalimbali ya walimu.

Hayo, yameelezwa na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama tarehe 27 Februari, 2025 alipokuwa katika Ofisi za TSC Wilaya ya Mkuranga ambapo alipata fursa ya kufanya kikao na Wajumbe wa Kamati ya Tume wa Wilaya hiyo.

Mwl. Nkwama alisema kuwa Wajumbe wa Kamati wanapaswa kupata nafasi ya kusoma nyaraka na kuzielewa kabla ya kuingia kwenye kikao cha kujadili na kufanya uamuzi kwa kuwa kazi yao ni nyeti na inagusa moja kwa moja maisha ya watumishi walimu.

Aliongeza kuwa, kila mjumbe ni lazima aelewe kwa undani kile anachokiamua na pale ambapo haelewi ni muhimu apatiwe majibu kabla ya kufikia hatua ya kufanya uamuzi.

“Wajumbe wa Kamati tunawategemea sana na maisha ya utumishi wa walimu yako mikononi mwenu. Hili ni jukumu kubwa sana, ajenda inapowekwa mezani ninaomba muitafakari kwa kina, pateni nafasi ya kupitia nyaraka kuona kama kila kitu kipo sawa na taratibu zote zimezingatiwa ndipo muamue,”

alisema Katibu huyo.

Aliongeza kuwa Kamati hiyo ipo huru na haiingiliwi na mtu yeyote katika kufanya maamuzi, hivyo aliwahimiza wajumbe kutokubali kushawisiwa au kushinikizwa bali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazowaongoza katika kufanya uamuzi.

“Tunajua mwalimu ana haki ya kukata rufaa Tume Makao Makuu kupinga uamuzi unaotolewa na Kamati ngazi ya Wilaya. Hivyo, Mwalimu anapokata rufaa Tume, ukipitiwa uamuzi uliotolewa na Kamati, kusiwe na dosari ya ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu katika uamuzi huo,” alisisitiza.

Aliongeza kuwa kupitia rufaa za walimu ilionekana kuwepo kwa dosari za mara kwa mara katika kuendesha mashauri ya nidhamu na kusababisha mashauri kurudishwa ili yakaanzishwe upya kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu jambo ambalo sio tu kwamba linasababisha hasara kwa serikali lakini pia linachelewesha haki kutendeka.

Kutokana na hilo, TSC iliamua kufanya mafunzo kwa wajumbe wa Kamati hizo nchi nzima kwa lengo la kuwaongezea uelewa wa sheria, kanuni na taratibu katika kuendesha mashauri ya nidhamu ya walimu.

“Kwa kuwa wajumbe mmepata mafunzo, lakini pia nyaraka zote zipo kwenye tovuti ya Tume, mtaendelea kujisomea na hatutarajii tena kuona dosari katika uendeshaji wa mashauri,” alisema Mwl. Nkwama.

Katibu huyo aliwapongeza Wajumbe Kamati hiyo ya Wilaya ya Mkuranga kwa kazi nzuri wanayofanya katika kushughulikia masuala mbalimbali ya walimu ikiwemo masuala ya ajira na maendeleo ya utumishi wa walimu na uendeshaji wa mashauri ya nidhamu.

Hata hivyo, Mwl. Nkwama aliwataka watumishi wa TSC katika Wilaya hiyo kuongeza kasi katika kufanya ziara shuleni ili kuwafikia walimu na kuwapa elimu juu ya masuala mbalimbali ya utumishi wao.

Kwa upande wa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mkuranga, Bi. Christina Ngalawa alisema kuwa Kamati hiyo imeendelea kutekeleza majukumu yake ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilipandisha vyeo walimu 332, mwaka 2023/2024 walimu 1171 walipandishwa ambapo 979 walipandishwa kawaida na walimu 192 walipandishwa baada ya zoezi maalum la kuhakiki walimu wenye changamoto za kupanda vyeo kufanyika.

Aliongeza kuwa, hadi kufikia mwezi Septemba, 2024 walimu 34 walikuwa wamebadilishiwa kazi/cheo huku akikiri kupokea maombi mapya ya walimu 137 wanaohitaji kubadilishiwa kazi/cheo ambapo alieleza kuwa kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa, maombi hayo yanashughulikiwa ili walimu waweze kubadilishiwa kazi/cheo.

“Mwezi huu (Februari, 2025) tumepokea walimu 69 wa ajira mpya ambapo walimu 12 ni wa shule za msingi na 57 ni wa shule za sekondari, walimu wote walisharipoti kwenye vituo vyao vya kazi. Aidha, kuanzia mwezi Julai hadi kufikia mwezi Februari, 2024 walimu watatu wamepewa vibali vya kustaafu.”

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya ya Mkuranga, Mwl. Josephine Ndonde alimshukuru Katibu wa Tume kwa kutembelea ofisi hiyo huku akiahidi kuwa Kamati yake itaendelea kufanya kazi kwa bidii ili walimu waweze kupata haki zao kwa wakati.

Pia, alisema Kamati hiyo itaendelea kuwaelimisha walimu ili kuwasaidia kuepuka kuingia katika ukiukwaji wa miiko na maadili ya utumishi wa walimu katika kutekeleza majukumu yao ili waweze kuongeza tija katika kutoa elimu kwa wanafunzi.

KAMATI ZA TSC ZA WILAYA ZATAKIWA KUONGEZA UFANISI WA UTENDAJI KAZI



Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Josephine Ndonde akizungumza wakati wa kikao cha Katibu wa TSC, Wajumbe wa Kamati na Watumishi wa Tume Wilaya ya Mkuranga tarehe 27 Februari 2025.



Mkurugezi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya akizungumza kwenye kikao cha Katibu wa Tume, Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo na Watumishi wa Tume Wilaya ya Mkuranga tarehe 27 Februari 2025.



Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mkuranga, Bi. Christina Ngalawa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC kwa Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na Watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga wakati alipofanya ziara katika ofisi za Tume Wilaya ya Mkuranga tarehe 27 Februari, 2025.



Baadhi ya Washiriki wa Kikao cha Katibu wa TSC na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga kikiwa kinaendelea.

KAMATI ZA TSC ZA WILAYA ZATAKIWA KUONGEZA UFANISI WA UTENDAJI KAZI



Baadhi ya Washiriki wa Kikao cha Katibu wa TSC na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga kikiwa kinaendelea.

PROF. MURUKE ATEMBELEA OFISI ZA TSC WILAYA YA RUFUJI, ATETA NA MKURUGEZI WA HALMASHAURI

Na Mwandishi wetu – Rufiji.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke tarehe 26 Februari, 2025 alifanya ziara katika Ofisi za TSC wilaya ya Rufiji kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.

Katika ziara hiyo aliyoambatana na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya pamoja na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Seksheni ya Maadili na Nidhamu, Mwenyekiti huyo alifanya kikao na Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya ya Rufiji na baadae alifanya kikao na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji.

Katika kikao chake na Kamati ya TSC, Prof. Muruke alipokea taarifa ya utekelezaji wa majuku ya TSC Wilaya ya Rufiji kutoka kwa Kaimu Katibu Msaidizi wa ofisi hiyo, Bi. Gloria Liwongwe ambaye alieleza kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Februari 2025 jumla ya walimu 372 walipandishwa vyeo.

"Tume imeendelea kupokea maombi ya walimu ya kubadilishiwa muundo ambapo maombi 33 ya walimu waliopanda vyeo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 yamewasilishwa kwa mwajiri kwa hatua ya utekelezaji. Aidha, Tume ilipokea na kusajili walimu 24 wa ajira mpya wa shule za Sekondari," alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Kwa upande wa usimamizi wa nidhamu, Bi. Gloria alieleza kuwa jumla ya mashauri tisa (9) ya nidhamu yalifunguliwa, kati ya hayo mashauri manne (4) yalihitimishwa kwa watuhumiwa kutopatikana na hatia, mashauri matatu yalihitimishwa kwa watuhumiwa kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi na mashauri mawili (2) bado hayajahitimishwa.

Naye Mwenyekiti wa Tume, Prof. Masoud Hadi Muruke aliwapongeza wajumbe wa kamati hiyo pamoja na watumishi wa TSC wa Wilaya ya Rufiji kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu wakati wa kuendesha mashauri ya nidhamu ambapo katika mashauri yaliyoamuliwa hakuna

rufaa iliyokatwa Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu.

"Ninawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya hususan katika kuendesha mashauri ya nidhamu. Ukiona umetoa adhabu na Mwalimu hakukata rufaa kupinga uamuzi uliotolewa maana yake ni kwamba ameona haki imetendeka. Hivyo, ninawasihi muendelea kufanya kazi kwa weledi kwa manufaa ya Taifa letu," alisema Prof. Muruke.

Hata hivyo, Prof. Muruke aliwataka wajumbe wa kamati pamoja na watumishi wa Tume wa Wilaya hiyo kujikita zaidi katika kutoa elimu kwa walimu ili kuwaepusha na ukiukwaji wa maadili ya kazi ya ualimu huku akisisitiza kuwa uwepo wa mashauri mengi sio kigezo cha kuonesha Tume inafanya kazi vizuri.

"Hatutaki TSC ionekane kuwa ni chombo cha kufukuza kazi walimu, lakini tunapaswa kuzuia walimu wasiingie kwenye makosa kwa kutoa elimu na ushauri. Hatupaswi kukaa kusubiri tu kushughulika na mashauri ya nidhamu, tukiwa na mashauri mengi tafsiri yake ni kwamba hatujatekeleza wajibu wetu vya kutosha," alisisitiza.

Naye Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa ni muhimu TSC na wasimamizi wengine wa elimu kama Maafisa Elimu, Maafisa Utumishi na Wathibiti Ubora wa Shule kupanga ziara za pamoja wanapokwenda kutembelea walimu shuleni ili kuhakikisha changamoto za walimu zinatatuliwa na elimu inatolewa ipasavyo.

Vilevile, Mwl. Nkwama alisisitiza watendaji wa TSC kutoa elimu kwa walimu waliojiendeleza kielimu ili pale wanapohitimu masomo yao wawasilishe maombi ya kubadilishiwa kazi/cheo ikiwa ni moja ya njia za kuondoa malalamiko ya walimu ya kucheleweshwa kubadilishwa cheo.

"Mwalimu anapomaliza masomo lazima tumpe elimu ili kama ana nia ya kubadilishiwa kazi/cheo basi afanye hivyo bila kuchelewa. Hivyo, ni muhimu sana kuimarisha mifumo ya mawasiliano kati ya TSC na walimu ili kutatua changamoto za walimu kwa wakati," alisema Mwl. Nkwama.

Katibu huyo alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kufanya mazoezi maalum ya kitaifa ya kuhakiki taarifa za walimu ili kubaini wale wenye changamoto na



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza wakati wa kikao chake na Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya ya Rufiji tarehe 26 Februari, 2025 katika ofisi za TSC Rufiji.

kuzitatu.

"Mwaka uliopita tulikuwa na zoezi la kitaifa la kupitia taarifa za walimu ambapo matokeo yake tuliona walimu wengi wakipandishwa vyeo kwa msereroko. Aidha, hivi karibuni imefanyika Samia Teachers' Mobile Clinic ambayo nayo imelenga kubaini walimu wenye changamoto mbalimbali ili zipatiwe ufumbuzi. Kwa kweli tunapongeza na kumshukuru Rais wetu kwa namna anavyojali walimu," alisema Mwl. Nkwama.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Tume, Prof. Muruke pamoja na ujumbe wake walipata nafasi ya kufanya kikao na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Bw. Simon Berege ambapo mwenyekiti huyo alimuomba kuweka kipaumbele katika kulipa madeni mbalimbali ya walimu.

Pamoja na hilo, Katibu wa Tume alimshukuru Mkurugenzi huyo kwa ushirikiano anaoutoa kwa Tume huku akisisitiza kuwa katika kushughulikia changamoto za walimu ni lazima Idara ya Utumishi na Idara za Elimu za halmashauri hiyo kufanya kazi kwa karibu na TSC.

Kwa upande wa Mkurugenzi huyo, Bw. Simon Berege alimshukuru Mwenyekiti wa Tume pamoja na ujumbe wake kwa kuamua kufanya ziara hiyo huku akiahidi kutekeleza mambo yote yaliyojadiliwa ili walimu waendeleo kuwa na mazingira bora katika kutekeleza majukumu yao.

PROF. MURUKE ATEMBELEA OFISI ZA TSC WILAYA YA RUFJI, ATETA NA MKURUGEZI WA HALMASHAURI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza wakati wa kikao kilichohusisha Mwenyekiti wa Tume na ujumbe wake na Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Rufiji tarehe 26 Februari, 2025 katika ofisi za TSC Wilaya ya Rufiji.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rufiji, Bi. Gloria Liwongwe akizwasilisha taarifa kwenye kikao kilichohusisha Mwenyekiti wa Tume na ujumbe wake na Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Rufiji tarehe 26 Februari, 2025 katika ofisi za TSC Wilaya ya Rufiji.



Kikao kilichohusisha Mwenyekiti wa Tume na ujumbe wake na Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Rufiji tarehe 26 Februari, 2025 katika ofisi za TSC Wilaya ya Rufiji kikiwa kinaendelea.



Picha ya pamoja kati ya Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC wakati wa ziara ya Mwenyekiti huyo na ujumbe wake katika ofisi za TSC Wilaya ya Rufiji tarehe 26 Februari, 2025.

Kikao kati ya Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (upande wa kulia) na ujumbe wake na Mkwurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Bw. Simon Berege (wa kwanza kushoto) kikiwa kinaendelea.

PROF. MURUKE ATEMBELEA OFISI ZA TSC WILAYA YA RUFJI, ATETA NA MKURUGEZI WA HALMASHAURI



Kikao kati ya Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke na ujumbe wake na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Bw. Simon Berege kikiwa kinaendelea.



Picha ya pamoja kati ya Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (Katikati), Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Bw. Simon Berege (wa pili kutoka kulia) pamoja na watumishi wengine wakati Prof. Mruke na ujumbe wake walipotembelea ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo tarehe 26 Februari, 2025.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Bw. Simon Berege akizungumza jambo wakati alipotembelewa na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke na ujumbe wake tarehe 26 Februari 2025.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Bw. Simon Berege wakati Prof. Muruke na ujumbe wake walipotembelea Mkurugenzi huyo ofisini kwake tarehe 26 Februari, 2026.

KATIBU TSC ATEMBELEA OFISI ZA TUME KISARAWA, APONGEZA UTARATIBU WA KUANDAA MPANGO KAZI

Na Mwandishi wetu – Kisarawe.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 27 Februari, 2025 alitembelea Ofisi za TSC Wilaya ya Kisarawe kwa lengo la kujionea namna ofisi hiyo inavyotekeleza majukumu yake katika kusimamia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu katika Wilaya hiyo.

Katika ziara hiyo, Katibu wa Tume aliambatana na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Seksheni ya Maadili na Nidhamu, Mwl. Asha Lubuva ambapo alipata fursa ya kuzungumza na baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Rufiji.

Mwl. Nkwama aliipongeza ofisi hiyo kwa kuandaa mpango kazi wa mwaka mzima unaoonesha ratiba ya utendaji kazi mbalimbali huku akieleza kuwa mpango kazi ni nyenzo muhimu inayosaidia kujipima kiutendaji.

"Ninawapongeza sana kwa kuwa na huu mpango kazi, hii ni nyenzo muhimu inayokupatia dira ya nini unatakiwa ufanye na kwa wakati gani. Ukishajiwekea mpango kazi ni rahisi kujipima na kuona kama unapiga hatua kwenda mbele au unarudi nyuma," alisema.

Mwl. Nkwama aliwataka watumishi hao kushirikisha Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe hususan Maafisa Elimu, Maafisa Utumishi pamoja na Wathibiti Ubora wa Shule ili wanapofanya ziara shuleni waende pamoja kutoa elimu na kutatua changamoto za walimu shuleni.

Akizungumzia shughuli za Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo, Mwl. Nkwama aliwataka wajumbe hao kuhakikisha taratibu zote zinazingatiwa hususan katika kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu ili kutenda haki.

"Ni lazima mjiridhishe kama taratibu zimezingatiwa na pale mnapoona kuna dosari msinyamaze mkaacha tu mambo yaende

hivyo hivyo. Mnapaswa kuhoji na kujiridhisha kabla ya kufanya uamuzi. Tukumbuke maamuzi tunayoyafanya yanabeba taswira ya Tume, kwa hiyo kama maamuzi yetu hayatakuwa ya haki tunasababisha Tume isiaminike," alisisitiza.

Katibu huyo aliwasisitiza watumishi wa Tume kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi katika kuhudumia walimu kwa kuwa azma ya Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuona changamoto za walimu zinatatuliwa ili waweze kuongeza tija katika kutoa elimu kwa wanafunzi.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya ya Kisarawe, Kaimu Katibu Msaidizi wa Wilaya hiyo, Bi Sophia Kizenga alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 walimu 756 walipandishwa vyeo, kati ya hao 427

ni wa shule za msingi na 329 ni wa shule za sekondari.

"Mwezi Februari, 2025 tulipokea walimu 15 wa ajira mpya, 10 wakiwa ni wa masomo ya biashara na watano (5) ni wa masomo ya sayansi kwa shule za sekondari," alisema.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa Wilaya ya Kisarawe ina jumla ya shule 113, za msingi zikiwa 91 na sekondari 22 huku idadi ya walimu ikiwa ni 1,401 ambapo wa shule za msingi ni 802 na sekondari ni 599.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo ya TSC Wilaya ya Kisarawe, Mwl. Allan Ngassa alimshukuru Katibu wa Tume kwa kuamua kutembelea wilaya hiyo huku akikiri kuwa ziara hiyo imewasaidia kujifunza mambo mengi ambayo yatawasaidia katika utekelezaji wa majukumu yao.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kisarawe alipofanya ziara katika ofisi hiyo tarehe 27 Februari, 2025.

KATIBU TSC ATEMBELEA OFISI ZA TUME KISARAWWE, APONGEZA UTARATIBU WA KUANDAA MPANGO KAZI



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kisarawe, Bi. Sophia Kizenga akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake kwa Katibu wa TSC wakati wa ziara ya Katibu huyo wilayani hapo tarehe 27 Februari, 2025.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu ya TSC, Mwl. Fatuma Muya akizungumza wakati wa kikao cha Katibu wa Tume, wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kisarawe tarehe 27 Februari, 2025.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Seksheni ya Maadili na Nidhamu, Mwl. Asha Lubuwa akizungumza wakati wa kikao cha Katibu wa Tume, wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kisarawe tarehe 27 Februari, 2025.



Kikao cha Katibu wa Tume, wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kisarawe kilichofanyika tarehe 27 Februari, 2025 kikiwa kinaendelea.

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kisarawe wakirwa kwenye hali ya utulivu wakati wa kikao cha Katibu wa Tume, wajumbe wa Kamati ya Ajira, Nidhamu na Upandishwaji Vyeo pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Kisarawe tarehe 27 Februari, 2025.

TSC KYELA YAIPONGEZA SERIKALI KWA KUSHUGHULIKIA MASLAHI YA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Kyela.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kyela imeishukuru Serikali kwa kushughulikia haki za walimu ikiwepo kupandishwa madaraja na kubadilishwa muundo kwa wakati.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume hiyo Wilaya ya Kyela, Bw. Julius Mwambogela wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini TSC.

“Kuanzishwa kwa Kliniki ya ufuatiliaji wa maslahi ya walimu kwa waliosaulika ili waweze kupata haki zao ni jambo lililofurahiwa na walimu wengi, na wengi walihudhuria kliniki hiyo ili kuweza kupata usaidizi wa kiutumishi, walimu wengi wanafikiri imekuwa mkombozi na mtatuzi wa changamoto zao,” alisema.

Bw. Mwambogela alisema kuwa TSC ni miongoni mwa wadau wanaoshirikiana katika kushughulikia migogoro na malalamiko na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya walimu.

Aidha, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuiwezesha fedha Tume kwa ajili ya utoaji mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali wanaosimamia walimu wilayani humo.

Bw. Mwambogela alisema kuwa kupitia uwezesaji huo wa Serikali waliweza kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati za Wilaya ambayo yamesaidia kutoa elimu ya uelewa wa pamoja kwa TSC na kazi zake na wajumbe wameelimishwa juu ya Sheria, Kanuni, Taratibu za kazi ya ualimu.

Alisema kuwa walitoa mafunzo kwa Wakuu wa Shule 107 ambayo yamesaidia kuleta matokeo chanya katika kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa walimu ambapo wakuu wa shule wameweza kuzijua Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu Utumishi wa Walimu.

Bw. Mwambogela alisema kuwa kupitia mafunzo hayo walimu wakuu wamejitambua kuwa wao ni miongoni



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume hiyo Wilaya ya Kyela, Bw. Julius Mwambogela akiendelea na majukumu yake.

mwa mamlaka za nidhamu, wametambua aina ya makosa (mepesi) ambayo yako ndani ya mamlaka yao, na yale mazito ambayo hayako kwenye mamlaka zao.

Bw. Mwambogela alisema kuwa kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela inajivunia kuwezesha kwa kupatiwa fedha za uendeshaji wa Ofisi, ukarabati na kuwa sehemu salama ya kutolea huduma.

Aliongeza kuwa Serikali katika Wilaya hiyo imeboresha miundombinu ya shule kupitia miradi ya BOOST na SEQUIP.

Wakati huo huo alisema kuwa jumla ya walimu 999 wamepandishwa vyeo katika Wilaya ya Kyela katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/2024 ambapo katika idadi hiyo walimu 563 walikuwa wa shule za msingi na 436 walikuwa wa shule za sekondari.

Aliongeza kuwa katika mwaka 2023/24 jumla ya walimu 65 walisajiliwa na kuthibishwa kazini ambapo wa Shule za Msingi walikuwa 26 na Sekondari 39.

Tume ya Utumishi wa Walimu katika Wilaya ya Kyela ina jumla ya walimu 1,622 ambapo Shule za Msingi ni 889 na Sekondari ni 733 ambao wanahudumia shule 138 ikiwa za Msingi ni 109 na Sekondari ni 29.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela, Bw. John Plasdus Danda akiendelea na majukumu yake.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kyela Augustino Mulabwa Laurent akiendelea na majukumu yake.

WALIMU WA SHULE YA MSINGI KILIMAHWEA WAMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUTATATUA CHANGAMOTO ZAO

Na Mwandishi wetu – Mafia.

Walimu wa Shule ya Msingi Kilimahewa iliyopo Wilaya ya Mafia mkoani Pwani wampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutatua changamoto zilizokuwa zinawakabili walimu kwa muda mrefu.

Pongezi hizo zimetolewa katika kikao kilichowakutanisha walimu hao na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke pamoja na Katibu wa Tume hiyo, Mwl. Paulina Nkwama wakati wa ziara yao shuleni hapo tarehe 24 Februari, 2025.

Akizungumza wakati wa kikao hicho, Mkuu wa Shule ya Msingi Kilimahewa, Mwl. Shelukindo Shekifu alisema kuwa Rais Samia amefanya kazi kubwa katika kuhakikisha maslahi ya walimu yanapewa kipaumbele jambo ambalo limefanya walimu kuendelea kufanya kazi kwa moyo.

“Tunaomba mtufikishie salamu zetu kwa Rais, kwa kweli kazi anayoifanya tunaiona, tunampongeza na kumshukuru sana kwa namna anavyotujali. Huko nyuma tulikuwa na malalamiko ya kutopanda vyeo, kutokubadilishiwa kazi/cheo lakini kwa sasa kila kitu kimekaa sawa,” alisema.

Aliongeza kuwa, “Madai mbalimbali ya walimu yameendela kulipwa, Mhe. Rais ameleta fedha nyingi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya shule na mambo mengi ambayo yanatuongezea morali ya kufanya kazi. Hata mnavyoona walimu hawana maswali ya kuuliza maana yake ni kwamba yale mambo mengi tuliyokuwa tunayapigia kelele sasa tumetekelezewa.”

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke alisema kuwa dhamira ya Serikali inayoongozwa na Rais Samia ni kufanya maboresho makubwa katika Sekta ya elimu ambapo maboresho hayo ni pamoja na kutatua changamoto za walimu ili waweze kutoa huduma bora ya kufundisha wanafunzi.

“Ujio wetu hapa ni sehemu ya



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke akizungumza katika kikao kilichowakutanisha Walimu wa Shule ya Msingi Kilimahewa iliyopo Wilaya ya Mafia wakati wa ziara ya Mwenyekiti huyo na ujumbe wake iliyofanyika shuleni hapo tarehe 24 Februari, 2025.

kutimiza azma ya Serikali katika kushughulikia masuala ya walimu. Katika watu wa kuangaliwa kwa jicho la pekee ni walimu, hii ni kutokana na majukumu yao wanayoyafanya, hakuna mtaalamu wala taaluma yeyote bila Mwalimu. Hivyo, tumekuja ili kuona yale mazuri ambayo Rais wetu ameyafanya pamoja na kuona changamoto ambazo bado

hazijatatuliwa ili tukazishughulikie,” alisema.

Naye Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama aliwapongeza walimu hao kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii jambo ambao limefanya ufaulu wa wanafunzi kuendelea kuongezeka huku akiwasihi kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kutekeleza majumu yao.

WALIMU WA SHULE YA MSINGI KILIMAHEWA WAMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUTATATUA CHANGAMOTO ZAO



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na walimu wa Shule ya Msingi Kilimahewa iliyopo Wilaya ya Mafia wakati wa ziara ya Mwenyekiti huyo na ujumbe wake iliyoifanyika shuleni hapo tarehe 24 Februari, 2025.



WALIMU WA SHULE YA MSINGI KILIMAHEWA WAMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUTATATUA CHANGAMOTO ZAO





TUME YA UTUMISHI WA WALIMU
THE TEACHERS' SERVICE COMMISSION

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu